

UFUATILIAJI WA TAKWIMU ZA VYANZO VYA VIFO KATIKA VIJJI VYENYE VIWANGO TOFAUTI VYA MAAMBUKIZI YA MALARIA WILAYANI KOROGWE

Ishengoma DRS, Kamugisha ML, Mmbando BP, Francis F, Gesase S na Lemnge MM

Taasisi ya Taifa ya utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Tanga, SLP 5004 Tanga, Tanzania

UTANGULIZI

Takwimu sahihi za vifo ni muhimu na hutumiwa katika kupanga mipango mbali mbali ya sekta ya afya, ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutathmini mafanikio ya mipango ya afya yenye lengo la kupunguza magonjwa na vifo. Hata hivyo takwimu hizo hazipatikani kirahisi katika nchi nyingi zinazoendelea kutokana na kutokuwa na mfumo sahihi wa kuhifadhi takwimu za vifo. Mbinu mbadala ijulikanayo kama verbal autopsy (VA) hutumika katika kutathmini vyanzo vya vifo katika maeneo yasiyo na takwimu rasmi. Kazi hiyo ya kutathmini ilianzishwa ndani ya mfumo wa ukusanayaji takwimu za sensa (DSS) katika vijiji 14 wilayani Korogwe kuanzia Januari 2006 ili kubainisha vyanzo vya vifo katika maeneo ya mradi kwa lengo la kutathmini mbinu mbadala za kudhibiti ugonjwa wa malaria.

KANUNI

Usaili unautumia utaratibu wa VA ulifanyika katika kaya zilizopata msiba; na kuhusisha wazazi au ndugu wa karibu wa marehemu. Majibu yaliyotolewa na wahusika yalifanyiwa uchambuzi na madaktari wawili hadi watatu ili kubainisha ugonjwa au kitu kingine kilicho sababisha kifo cha marehemu.

MATOKEO

Vifo 554 vilitokea katika eneo la utafiti kuanzia Januari 2006 hadi Juni 2008. Usaili ulihusisha matukio 333 (60.1%) na uchambuzi uliofanywa na madaktari uliwezesha kujua chanzo cha vifo 280 (84.1%). Vifo 216 (64.9%) vilitokea nyumbani na vifo 53 (35.1%) ndivyo vilitokea hospitali au zahanati/ kituo cha afya. Magonjwa ya kuambukiza (CDs) ndiyo yalisababisha vifo vingi (vifo 146, 43.8%), yakifuatiwa na magonjwa yasiyoambukiza (vifo 98, 29.4%) kama inavyooneshwa kwenye umbo Na. 1. Kati ya vyanzo vyote, malaria na ukimwi viliongoza kwa kusababisha vifo vingi katika eneo la utafiti. Kati ya magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya moyo na kansa yalisababisha vifo vingi na hasa kwa watu wazima kuanzia miaka 45 (Umbo Na. 2).


HITIMISHO

Vifo vingi vilivyotokea katika eneo la mradi vilitokea nyumbani, nje ya hospitali. Malaria na Ukimwi (HIV/AIDS) magonjwa yaliyosababisha vifo vingi, kwa watoto wadogo na watu wazima kuanzia miaka 15-44. Hata hivyo kwa watu wazima wenye umri zaidi ya miaka 45, vifo vingi vilisababishwa na magonjwa yasiyoambukiza (magonjwa ya moyo na kansa). Kwa hiyo mipango ya kudhibiti magonjwa na vifo katika maeneo haya vinatakiwa kuzingatia taarifa hizi ili mbinu zitakazobuniwa ziweze kulenga magonjwa yanayoathiri rika hizo. Hata hivyo tunakabiliwa na upungufu wa fedha ili kuifanya kazi hii iwe endelevu.


SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wakazi wote wa eneo la mradi kwa kufanikisha kazi hii. Tunawashukuru wafanyakazi wote wa Kituo cha Tanga walioshiriki katika kazi hii kwa msaada wao. Pia tunaashukuru uongozi wa Wilaya ya Korogwe na NIMR makao makuu kwa msaada wao. Kazi hii imefadhiliwa na African Malaria Network trust (AMANET) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na: DRS Ishengoma; dishengoma@tanga.mimcom.net (027 264 7957).



Umbo Na. 1: Vyanzo vya vifo katika maeneo ya mradi



Umbo Na. 2: Magonjwa yaliyosababisha vifo kwa watu wazima miaka 45+